

Maswali

1. Mbona Waisraeli walilalamika tena?
2. Nani aliamini Mungu?
3. Mungu aliambia Musa afanye nini?
4. Mbona Musa alikasirika?
5. Musa alifanya nini?
6. Nini kilitoka kwa mwamba?
7. Mbona Mungu hakufurahia Musa?
8. Mungu aliadhibu Musa namna gani?
9. Kwa hii hadithi Mungu anatufundisha nini?
10. Musa aliharibu hilo funzo namna gani?

Majibu

1. Waisraeli walikuwa na kiu. Hawakuwa na maji.
2. Musa na Haruni waliamini Mungu.
3. Mungu aliambia Musa ashike fimbo na azungumze na mwamba.
4. Musa alikasirika kwa sababu Waisraeli hawakuamini Mungu.
5. Musa alipiga mwamba mara mbili.
6. Maji yalitoka kwa mwamba.
7. Musa hakuamini kabisa alivyoamriwa na Mungu.
8. Musa hakukubaliwa kuingia kwa nchi ya ahadi.
9. Mwamba ni wa nguvu na haubadiliki, uwezo wa Yesu ni wa nguvu, upendo wake haubadiliki. Mwamba ulipigwa kuleta uzima.
10. Musa aliharibu hili funzo kwa kupiga mwamba .

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



5 Musa anapiga mwamba

Marejeo

Hesabu 20: 2 – 13.

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima tumtii Mungu sawasawa.

Maneno maalum

1. Waisraeli + kiu + nung'unika
2. Amini Mungu + fimbo + nena + nyingi
3. Kasirika + paza sauti + piga mara mbili
4. Maji mengi
5. Hakufurahia + hakuna utukufu kwa Mungu
6. Zungumza sio piga
7. Adhibu + hakuna nchi ya ahadi
8. Ona nchi + kifo + ufufuo.
9. Tii Mungu + soma somo
10. Mwamba ni Yesu+ kufa mara moja.

5.1 Waisraeli walisafiri kwenda bara la Sini. Na hawakukuwa na maji ya kunywa. Punde tu wakawa na kiu. Walianza kumnungu'nikia Musa na Haruni wakisema, "Mbona mmetuleta kwa hili jangwa? Tutakufa hapa. Tulipokuwa Misri tulikuwa na matunda ya kula na hata maji ya kunywa. Tutakufia hapa pahali pabaya."

5.2 Musa na Haruni waliamini Mungu. Walienda maskani katikati ya kambi. Utukufu wa Mungu uliwatokea. "Akawaambia shika fimbo yako, na uzungumzie huu mwamba. Amrishe maji yatoke kwa huo mwamba. Maji mengi yatatoka na kila mtu atakunywa."

5.3 Musa akachukua fimbo na kukusanya Waisraeli wote pamoja. Musa aliwakasirikia kwa sababu hawakuamini Mungu tena. Musa alipaza sauti ya hasira, "Sikiliza enyi waasi tuwatolee maji katika mwamba huu?" Musa alikuwa na hasira na uoga pia. Alijua hao watu wangempiga kwa mawe asipowapa maji. Kwa hivyo akapiga mwamba mara mbili kuhakikisha maji yametoka.

5.4 Punde tu Musa alipopiga mwamba maji yalimwagika nje. Yalitiririka chini ya mwamba. Watu wote walikunywa na kufarahia.

5.5 Mungu hakufurahia Musa. Musa alisema, "Lazima sisi tuwape maji kutoka kwa huu mwamba?" Hakuwa Musa aliyewapa maji. Alikuwa Mungu. Musa hakumtukuza Mungu kwa kuwapa maji.



5.6 Musa hakutii Mungu kabisa. Mungu alimwambia Musa **ASEME** na mwamba. Musa hakuamini Mungu sana. Hakutii Mungu kabisa. Musa **ALIPIGA** mwamba mara mbili badala ya kunena nao.

5.7 Kwa sababu Musa hakutii amri za Mungu kabisa aliadhibiwa. Mungu alimwambia Musa kwamba hatakubaliwa kwenda kwa nchi ya ahadi. Musa hakufurahi. Aliwaongoza Waisraeli jangwani kwa miaka arobaini, lakini hakukubaliwa kuingia kwa nchi ya ahadi.

5.8 Mungu alipeleka Musa kwa mlima mrefu ili aone nchi kabla afe. Lakini hakukubaliwa kwenda kwa hiyo nchi. Tunajua kwamba Yesu atakaporudi hapa duniani, atafufua Musa kutoka kwa wafu. Ufalme wa Mungu utakapokuja hapa duniani, Musa ataingia kwa nchi ya ahadi na aishi humo. Musa hakukubaliwa kwenda kwa nchi kwa sababu hakutii amri za Mungu kabisa.

5.9 Hadithi hii inatuonyesha vile ni jambo la mhimu kila wakati tutii Mungu kabisa. Katika Agano la kale, Mungu anatumfundisha mengi sana yatakayokuwako Yesu akija. Mungu alikuwa anatuonyesha juu ya Yesu lakini Musa akaharibu hilo somo kwa kupiga mwamba tena. Musa alikuwa amewahi kupiga mwamba liwatolee watu maji wanywe huko Refidimu. Mara hii Mungu alitaka azungumze na mwamba tu.

5.10 Mwamba ni mgumu hauwezi kubadilika. Yesu ni kama mwamba. Uwezo wa Yesu ni wa nguvu. Upendo wake kwetu haubadiliki. Maji yanatupa uzima. Bila maji tungekufa. Yesu mwamba wetu alisulubiwa kutupa tumaini la uzima wa milele. Yesu alikufa mara moja. Hili funzo liliharibiwa na Musa kwa kupiga mwamba tena.